



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MKUTANO WA KIMATAIFA WA ELIMU BORA, 18-20 MEI 2021, DAR ES SALAAM

Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET) ni mtandao unaoundwa na Asasi za Kiraia (AZAKI) 140 zinazofanya kazi katika sekta ya elimu Tanzania Bara tangu 1999 kwa madhumuni ya kutetea upatikanaji wa elimu jumuishi na bora kwa wote.

Kila mwaka TEN/MET huandaa Mkutano wa Ubora wa Elimu ambao hutoa fursa kwa wadau wa elimu ikiwepo serikali, wanachama wa mtandao, Washirika wa Maendeleo (Development Partners) pamoja na wadau mbalimbali wa elimu hapa nchini kujadili hali ya ubora wa elimu kwa nia ya kuboresha utoaji wake hapa nchini. Mwaka huu mkutano huo umeandaliwa kwa kuchukua taswira ya kimataifa ili kutoa fursa ya kujifunza na kubadilishana uzoefu wa namna ya kuweka mikakati ya kuimarisha ubora wa Elimu baina ya nchi moja na nyingine. Mkutano huu utafanyika Dar es Salaam kwenye ukumbi wa Kisenga uliopo jengo la LAPF tower Makumbusho kuanzia tarehe 18 hadi 20 Mei 2021.

Mada kuu ya mkutano huu ni **Uwajibikaji wa pamoja katika kugharamia elimu bora**. Mada hii itaelezewa vizuri na mgeni rasmi. Zipo mada nyingine kumi na tano zitakazojadiliwa kwa muda wa siku tatu za Mkutano; na mada zote zimelewa katika kuboresha elimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Mkutano huu utahudhuriwa na wajumbe kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, TAMISEMI, Mashirika yasiyo ya kiserikali, Wadau wa maendeleo, waheshimiwa Wabunge, Taasisi za elimu ya juu, tasisi za utafiti, Vyuho na shule za ufundi, Walimu, Wazazi na Wanafunzi. Aidha mkutano huu utahudhuriwa pia na mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao, wageni wengine mbalimbali kutoka nchi za ng'ambo, makampuni na taasisi za watu binafsi. Wajumbe takriban 200 wamethibitisha kushiriki katika mkutano huu; baadhi watakuwa wakishiriki kwa njia ya Mtandao.

Mgeni rasmi wa mkutano huu ni Mheshimiwa Daktari Jakaya Mrisho Kikwete, Raisi Mstaafu wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kamishina wa Kamisheni ya Elimu inayoundwa na umoja wa Mataifa.

Aidha, Mkutano huu unatarajiwa kutoka na maazimio ambayo ni mapendekezo ya namna ya kutatua changamoto mbali mbali zinazoikabili sekta ya elimu hapa nchini kwa kutumia matokeo ya taarifa za tafiti na uzoefu kutoka nchi nyingine.

Maandalizi yote ya mkutano huu yamekamilika na nichukue fursa hii kuwashukuru wadau mbalimbali ambao wamewezesha kufanyika kwa Mkutano. Kwa namna ya pekee niwashukuru wenzetu wa ubalozi wa Swedeni kwa msaada wao ambao umewezesha kwa kiwango kikubwa kufanikisha Mkutano huu. Niwashukuru pia Global Partnership for education kupitia mradi wa Education Out Loud, Norad kupitia ActionAid Tanzania, Pestalozzi na HDIF Tanzania. Lakini pia TEN/MET inapenda kuwashukuru washiriki wote hasa waliolipia ada ya ushiriki hivyo kufanya mkutano wetu ufikie malengo yake.

Tunapenda kutoa taarifa kuwa wote waliokosa fursa ya kuja kwenye mkutano huu watufuatilie kupitia njia ya mitandao yetu ya kijamii ili kujifunza na kuchangia kwa njia ya mtandao kwani michango mizuri tutaiweka kwenye taarifa yetu itakayoenda kwa serikali Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekinolijia na Tamisemi.

Mwisho nitowe wito kwenu waandishi wa habari na vyombo vya habari kuendelea kutoa habari za mwendeleo wa Mkutano huu ili kuwapelekea wananchi majadiliano muhimu ya namna ya kuboresha ubora wa elimu hapa nchini. Hii itakuwa fursa ya kipekee kuweza kujadili namna ya kuboresha mfumo wetu wa elimu sawa na wito uliotolewa na Raisi Wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu hivi karibuni.

Asanteni sana kwa kunisikiliza. Sasa nakaribisha maswali

Ochola Wayoga
Mratibu wa Taifa TEN/MET
16 Mei 2021

-----Mwisho-----